TANGAZO LA SERIKALI NA. 511 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote chenye thamani kinachopelekwa sokoni kwa madhumuni ya kuuzwa;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au mnyama anayetumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi

inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa au madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"maegesho maalumu" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri na kubainishwa kutumika kwa ajili ya kuegesha magari chini ya uangalizi maalumu wa Halmashauri, na inajumuisha eneo la Nyerere square, pamoja na maeneo ya taasisi yaliyoombewa kibali;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"masoko" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"utamaduni" maana yake ni sanaa za maonesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, ususi, michezo, muziki wa dansi, video, muziki wa taarabu, maonesho ya sinema, mazingaombwe, tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"Wakala" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, shirika au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru

kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayepaswa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku, kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kwza kuzingatia makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ushuru wa huduma

7.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa

huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu ya mauzo baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii kutoka kwa mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye hawasilishi hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(3) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye anawajibika kulipa ushuru wa huduma atapaswa kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa za hesabu za mwaka kwa ajili ya kukokotoa kiwango.

(4) Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa ushuru wa huduma katika kipindi maalumu cha hesabu.

(5) Mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa ushuru wa huduma si zaidi ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa

kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo za (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kuwa Wakala kwa madhumuni ya kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na
(c) kutouza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Mkurugenzi.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kamati ya Mapato

11.-(1) Kutakuwa na Kamati ya kufatilia mapato ya

Halmashauri itakayoundwa na Mkurugenzi ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu utendaji kazi wa kikosi kazi cha kukusanya mapato;

(b) kuishauri Halmashauri kuhusu namna ya kuongeza mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato; na

(c) kufanya tathmini ya makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka ili kuweka maoteo ya mwaka unaofuata.

(2) Kamati ya mapato itawajibika kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa Menejimenti kila mwezi kuonesha namna ilivyofanya kazi katika kipindi husika.

Kikosi kazi cha kudhibiti Mapato

12.-(1) Kutakuwa na kikosi kazi cha kufuatilia na kudhibiti utoroshaji wa mapato ambacho kitaundwa na Mkurugenzi kikihusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali za Halmashauri.

(2) Kikosi kazi kitakachoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kitawajibika kwa Kamati ya Mapato.

Makosa

13. Mtu anatenda kosa ikiwa -

(a) anashindwa, anadharau, anakwepa au anakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) anamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) anamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) anatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) anatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au

(f) anatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

14. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS.Na. 674 la 2020

16. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto za Mwaka 2020 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))

SEHEMU YA KWANZA

Ada ya ukaguzi wa Ramani za Majengo na Utoaji Vibali vya Ujenzi.

Namba	Ukubwa wa kiwanja	Kiasi cha ada (Shilingi)
1.	Nyumba za makazi kwenye Kiwanja kikubwa	50,000/=
2	Nyumba za makazi kwenye Kiwanja cha kati	40,000/=
3	Nyumba za makazi kwenye kiwanja kidogo	30,000/=
4	Viwanda, mahoteli na nyumba za kulala wageni bila kujali ukubwa wa kiwanja	100,000/=
5	Jengo la ghorofa kwa kila sakafu bila kujali ukubwa wa kiwanja	100,000/=
6	Majengo mengine (mfano maduka, maeneo ambayo hayajapimwa)	50,000/=

Makao Makuu ya Wilaya	Kwa shughuli za makazi		Kwa shughuli za viwanda na biashara	Kwa huduma za kijamii
	0-400 mita za mraba	Zaidi ya 4000 mita za mraba		
	Kila mita ya mraba 1360/=	Kila mita ya mraba 4240/=	Kila mita ya mraba 2,800/=	Kila mita ya mraba 720/=
Maeneo nje ya Makao Makuu ya Wilaya	Kila mita ya mraba 720/=	Kila mita ya mraba 1,920/=	Kila mita ya mraba 1,920/=	Kila mita ya mraba 400/=
Minara ya simu	400,000/=Kila mnara			

SEHEMU YA PILI

Ushuru wa Vyombo vya Usafiri vinavyoingia katika
Magulio, masoko na minada ya Halmashauri.

Na.	Aina na uwezo wa gari	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Gari la zaidi ya abiria 39.	2,000 kwa siku
2.	Gari la abiria 20-39	1,500/= kwa siku
3.	Gari dogo la abiria chini ya abiria 20	1,000/= kwa siku
4.	Teksi	500/= kwa siku
5.	Magari binafsi yasiyo ya biashara	500/= kwa siku
6.	Gari dogo la mizigo [pikapu au lori chini ya tani 7]	2,000/= kwa siku
7.	Gari kubwa zaidi ya tani 7	2,500/= kwa siku
8.	Piki piki (boda boda)	500/= kwa siku.
9.	Mikokoteni ya aina yote	300/= kwa siku.

SEHEMU YA TATU

Ada ya Ukaguzi wa mifugo na nyama

Na.	Aina ya mfugo	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Ng'ombe	3,500/= kwa ng'ombe mmoja
2.	Mbuzi	2,000/= kwa mbuzi mmoja
3.	Kondoo	2,000/= kwa kondoo mmoja
4.	Nguruwe	3,500/= kwa nguruwe mmoja

SEHEMU YA NNE

Ada ya kibali cha kufanya biashara ya mazao ya misitu

Namba.	Aina ya zao	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Mkaa	300,000 kwa mwaka
2.	Mbao	1,000,000/= kwa mwaka
3.	Kuni	100,000/= kwa mwaka
4.	Nguzo	100,000/= kwa mwaka
5.	Fito	100,000/= kwa mwaka
6.	Kukata au kuvuna mti	1,000/= kwa mti mmoja

SEHEMU TANO

Ushuru wa Mazao ya Misitu

Namba	Aina ya bidhaa	Ujazo	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Mbao za miti laini	2*2	200
		2*3	200
		2*4	200
		2*5 na zaidi	300
		1*8 na zaidi	300
2.	Mbao za miti migumu	2*2	400
		2*3	400
		2*4	400
		2*5 na kuendelea	500
		1*10 na zaidi	500
3.	Magogo ya miti migumu	kila gogo moja	3000
4.	Magogo ya miti laini	kila gogo moja	2000
5.	Nguzo za umeme	DHB 20-30	3000
6.	Mapau	10 – 15 cm	500
7.	Fito	mzigo (fito 50)	50
8.	Reject	-	200
9.	Mkaa	kila gunia	2000
10.	Miche ya niti ya	mche mmoja	30

	mapambo		
11.	Miche ya kawaida	mche mmoja	25
12.	Slabs na mabanzi		100
13.	Milunda/mapuu		300

SEHEMU YA SITA

ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI, UKAGUZI WA AFYA NA USAJILI WA VIKUNDI

(i) ADA YA KUKODI UKUMBI

Namba.		Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Ukodishaji ukumbi kwa ajili ya shughuli za mashirika na miradi.	100,000 kwa ukumbi mdogo na 200,000 kwa ukumbi mkubwa
2.	Kukodisha viti	500/= kwa kiti
3	Tahadhari (inayorejeshwa kama hakuna uharibifu wa ukumbi au upotevu wa mali za halmashari ukumbini)	100,000/=

(ii) ADA YA KUKODI MAGARI NA MITAMBO

1.	Ada ya kukodi gari	Kama itakavyoamuliwa na Halmashauri kutegemeana na gharama za umbali, gharama za mafuta na matumizi ya mkodishaji na muda wa gari kukodishwa.
2.	Ada ya kukodi mashine/mtambo	Kama itakavyoamuliwa na Halmashauri kutegemeana na gharamana na aina ya mashine na muda wa mkodishaji kutumia.

(iii) ADA YA UKAGUZI WA AFYA

Na.	Eneo	kiasi cha ushuru
1.	Nyumba za starehe, baa na vilabu vya pombe za kienyeji	10,000/= kila baada ya miezi 6
2.	Nyumba za kulala wageni	10,000/= kila baada ya miezi 6
3.	Maduka ya bidhaa	10,000/= kila baada ya miezi 6
4.	Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma	10,000/= kila baada ya miezi 6
5.	Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara	10,000/= kila baada ya miezi 6
6.	Ukaguzi wa viwanda vikubwa	100,000/= kila baada ya miezi 6
7.	Ukaguzi wa viwanda vya kati na karakana	50,000/= kila baada ya miezi 6
8.	Ukaguzi wa viwanda vidogo	20,000/= kila baada ya miezi 6
9	Mama ntilie na magenge ya aina yote	5,000/= kila baada ya miezi 6.
10.	Masuala ambayo hayajatajwa na yanahitaji ukaguzi	3,000/= kila baada ya miezi 6

SEHEMU YA SABA

Ada ya Ushuru wa soko

Na.	KIASI	MUDA
1.	TSHS 500	KWA SIKU

`

SEHEMU YA NANE

Ushuru wa Madini ya Ujenzi.

Namba	Uzito wa gari	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Tani 1 hadi 3 kwa trip	4,500/=

2.	Tani 4 hadi 7 kwa Trip	10,000/=
3.	Tani 8 hadi 10 kwa Trip	15,000/=
4.	Tani 11 na 12 kwa Trip	20,000/=
5.	Tani 12 nakuendelea	25,000/=

SEHEMU YA TISA

Ada ya shughuli za utamaduni;

Namba.	Aina ya shughuli	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Disko siku za sikukuu au siku yoyote ya mapumziko.	20,000/= kwa mwaka
2.	Michezo na sanaa za maonyesho, ngoma, sarakasi, michezo ya kuigiza.	10,000/= kwa mwaka
3.	Shughulizasanaazaufundi /uchoraji, picha za rangi na vinyago.	10,000/= kwa mwaka
4.	Kucheza meza za pool.	20,000/= kwa mwaka
5.	Kuendesha promotion katika baa au hotel au eneo la wazi.	25,000/= kwa mwaka
6.	Shughuli za harusi na sherehe nyinginezo.	15,000/= kwa mwaka
7.	Video au sinema kwa siku	2,000/= kwa mwaka
8.	Waganga wa Jadi	10,000/= kwa mwaka
9.	Wauzaji wa dawa za kienyeji	15, 000/= kwa mwaka
10.	Shughuli yoyote katika eneo la Kijamii itakayohitaji kufunga matumizi ya kijamii	30,000/= kwa siku
11.	Shughuli yoyote isiyotajwa hapo juu.	10,000/= kwa mwaka

SEHEMU YA KUMI

A: Kodi ya nyumba za biashara za Halmashauri.

NA.	DARAJA	AINA YA KODI	KIASI
1.	A	KODI YA PANGO	250,000 KWA MWEZI
2.	B	KODI YA PANGO	200,000 KWA MWEZI
3.	C	KODI YA PANGO	150,000 KWA MWEZI
4.	D	KODI YA PANGO	100,000 KWA MWEZI
5.	E	KODI YA PANGO	50,000 KWA MWEZI

B: Kodi ya Nyumba Zilizojengwa Kwenye Ardhi Ya Halmashauri

NA	MAHALI	KIASI
1.	Lushoto mjini	50,000 kwa mwezi
2.	Nje ya mji	30,000 kwa mwezi

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Vituo vya vyombo vya usafiri

Na.	Jina la kituo	Kata
1.	Stendi Kuu	Lushoto
2.	Stendi Kuu	Mnazi
3.	Stendi Kuu	Mlalo
4.	Stendi Kuu	Mlola
5.	Stendi Kuu	Mtae

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ushuru wa chombo cha usafiri

Tangazo la Serikali Na.511 (Linaendelea.)

Namba.	AINA YA CHOMBO	GHARAMA YA KUTUMIA (inatozwa kila chombo kinapoingia/kutoka)
1.	Basi kubwa	3,000/=
2.	Basi la kati	2,500/=
3.	Basi dogo	2,000/=
4.	Mabasi mengine/Jamii ya daladala	1,500/=
5.	Teksi	1,000/=
6.	Tipa	2,500/=
7.	kenta	2,000/=
8.	Pikapu	1,500/=
9.	Magari mengine	3,000/=
10	Bajaji/Guta (Pikipiki za miguu 3)	500/=
11	Pikipiki	300/=

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ada ya kutoa huduma za kutembeza wageni pamoja na kutembelea vivutio vya asili

Namba	Aina ya shughuli	Kiasi cha Ushuru (Shilingi)
1.	Ada ya kibali cha kuongoza watalii	50,000/= kwa mwaka
2.	Tozo ya kutembelea vivutio vya asili kwa mtalii mtanzania	kwa kila eneo la kivutio; 2000/= (mtu mzima) 500/= (wanafunzi) Bure kwa watoto chini ya miaka 5
3.	Tozo ya kutembelea vivutio vya asili kwa mtalii asiye Mtanzania	kwa kila eneo la kivutio; 5000/= Bure kwa watoto chini ya miaka 5

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Lushoto, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YA HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..……………………......
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imebandikwa katika hizi Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kufuatia Azimio la kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kilichofanyika tarehe 12/5/2023 na kushuhudiwa,

Lakiri imebandikwa mbele ya:-

IKUPA H. MWASYOGE,
Mkurungenzi mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
Lushoto

MATHEW MBARUKU,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya wilaya,
Lushoto

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi,